

**CAPITAL
DEVELOPMENT
AUTHORITY
P.O. BOX 1 & 913
DODOMA**



**MAMLAKA
YA USTAWISHAJI
MAKAO MAKUU
S.L.P 1 & 913
DODOMA**

Telephone +255 26 2324053 / 2321569 Fax +255 26 2323248 / 2322650 E mail Info @ cda.go.tz website www.cda.go.tz

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UPATIKANAJI WA VIWANJA KWA WATUMISHI WA SERIKALI WANAOHAMIA MAKAO MAKUU YA NCHI DODOMA

Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (CDA) Dodoma inawatangazia watumishi wote wa umma wanaohamia Dodoma kuacha kununua viwanja visivyopimwa kupitia madalali ili kuepukana na utapeli unaoendelea hivi sasa.

Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (CDA) imeandaa utaratibu wa kuwamilikisha viwanja watumishi wote wa Serikali wanaohamia Dodoma, zoezi ambalo litaanza hivi karibuni.

Watumishi wote wanatakiwa kuwasilisha maombi ya viwanja kupitia kwa Wakurugenzi wa Utawala na Rasilimaliwatu waliopo katika Wizara zao, Idara na taasisi za Serikali, kwa kuwa utaratibu wa ukubwa wa viwanja pamoja na gharama za kulipia walishaelekezwa.

Aidha Mamlaka inawakumbusha wale wote walioandika barua za kuomba viwanja mara baada ya kutangazwa kwa Serikali kuhamia Dodoma kuzipitisha kwa Wakurugenzi wa Utawala na Rasilimaliwatu.

Mamlaka inapenda kuwakumbusha Watumishi wote wa Serikali kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji Namba 8 ya mwaka 2007 ni makosa kufanya shughuli za uendelezaji miji ikiwemo ujenzi wa aina yoyote bila ya kuwa na kibali kutoka kwa Mamlaka husika.

Imetolewa na


Angela Msimbira

Kaimu Meneja Uhusiano

MAMLAKA YA USTAWISHAJI MAKAO MAKUU

P.O.BOX 913

DODOMA

20/04/2017

Correspondence should be addressed to the Director - General